**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**OFISI YA RAIS-FEDHA NA MIPANGO**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBA 2023/2024

**NOVEMBA, 2023**

# YALIYOMO


**UTANGULIZI** ..... 2

**1.0 MWENENDO WA HALI YA UCHUMI JULAI-SEPTEMBA 2023** ..... 2

1.2 Uchumi wa Zanzibar ..... 2

1.3 Hali ya Mfumko wa Bei ..... 3

1.3.1 Mfumuko wa Bei wa Dunia ..... 3

1.4 Uingiaji wa Watalii ..... 4

1.5 Mwenendo wa Thamani ya Sarafu ya Tanzania ..... 5

1.6 Uingizaji na Usafirishaji wa Bidhaa ..... 6

1.7 Hali ya Chakula ..... 7

1.8 Hali ya upatikanaji wa ajira ..... 8

**2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI JULAI-SEPTEMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** ..... 8

2.1 MAPATO YA SERIKALI ..... 8

2.1.1 Mapato ya ndani ..... 9

i. Mapato kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ..... 9

ii. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Upande wa Zanzibar ..... 9

iii. Mapato yasiyokuwa ya kodi ..... 9

2.2 Mapato Mengineyo ..... 10

2.2.1 Mapato ya Washirika wa Maendeleo ..... 10

2.2.2 Mikopo ya Ndani ..... 11

2.3 MATUMIZI YA SERIKALI ..... 11

2.3.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida ..... 12

2.3.2 Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ..... 13

2.3.2 Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ..... 13

2.4 Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ..... 14

**3.0 UTEKELEZAJI MPANGO WA MAENDELEO JULAI – SEPTEMBA 2023** ..... 14

3.1 Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele kwa Kipindi cha Julai- Septemba 2023 ..... 14

3.1.1 Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu ..... 15

3.1.2 Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii ..... 19

3.1.3 Utawala bora na Uhimilivu ..... 21

3.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai - Septemba 2023/2024 ..... 22

3.3 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2023/24 ..... 22

**4.0 DENI LA TAIFA** ..... 23

**5.0 HITIMISHO** ..... Error! Bookmark not defined.

**6.0 VIAMBATISHO** ..... 26

## UTANGULIZI

Taarifa hii ya utekelezaji wa robo ya kwanza Julai – Septemba 2023/2024 inawasilishwa kwa pamoja na taarifa zifuatazo.

i. Taarifa za Mwenendo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar,

ii. Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, mapato na matumizi kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023

iii. Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai-Septemba, 2023 na

iv. Mwenendo wa Deni la Taifa

## 1.0 MWENENDO WA HALI YA UCHUMI JULAI-SEPTEMBA 2023


### 1.1 Ukuaji wa Uchumi Afrika Mashariki

Uchumi wa nchi za Afrika Mashariki kwa kipindi cha robo ya kwanza umekua kwa kasi, hadi kufikia asilimia 5.6 nchini Kenya, Uganda asilimia 6.5 na Tanzania asilimia 5.3 kwa mwaka 2023.

### 1.2 Uchumi wa Zanzibar

Katika robo ya kwanza 2023, Pato la Taifa kwa bei za soko (current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 1.5 trilioni ikilinganishwa na TZS 1.4 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Pato Halisi la Taifa kwa bei za kudumu (constant price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 906.3 bilioni mwaka 2023 ikilinganishwa na TZS 853.6 bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Hii ni sawa na ukuaji wa uchumi wa wastani wa asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na ukuaji wa sekta ndogo zikiwemo za biashara za jumla na rejareja (asilimia 16.1), ufugaji (asilimia 12.1), Ujenzi asilimia (10.9), ukodishwaji wa majengo (asilimia 7.2) na bidhaa za kodi (asilimia 6.9) na sekta nyengine ndogo kama inavyoonekana kwenye mchoro.

**Mchoro namba 1: Mchango wa sekta katika Pato la Taifa katika robo ya kwanza 2023**




**Chanzo:** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## 1.3 Hali ya Mfumko wa Bei

### 1.3.1 Mfumuko wa Bei wa Dunia

Kasi ya mfumko wa bei Duniani kufikia Septemba mwaka 2023 imeendelea kupungua na kufikia asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 8.7 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.


### 1.3.2 Mfumko wa Bei Zanzibar

Kwa kipindi cha Julai–Septemba mwaka 2023, kasi ya mfumko wa bei Zanzibar, imeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 6.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa bei za bidhaa za chakula kama vile (mchele (mapembe) kutoka TZS 1,733 mwaka 2022 kufikia TZS 2,229 mwaka 2023; sukari (*brown*) kutoka TZS 2,197 mwaka 2022 kufikia TZS 2,842 mwaka 2023; unga wa ngano kutoka TZS 1,921 mwaka 2022 kufikia 2,101 mwaka 2023; na ndizi mbichi kutoka TZS 1,467 mwaka 2022 kufikia TZS 1,793 mwaka 2023). Mfumko wa bei kwa bidha za chakula umefikia wastani wa asilimia 12.7 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2022.

Kasi ya mfumko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula kwa kipindi cha Julai-Septemba imepungua kufikia wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2023 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2022.

Sababu za kuongezeka kasi ya mfumko wa bei ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji, kuongezeka kwa thamani ya Dola ya Kimarekani dhidi ya Shilingi ya Tanzania na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za ndani za chakula kutokana na kupungua kwa eneo la uzalishaji na wananchi kuhamasika kwa kulima kilimo cha mboga mboga ambacho mavuno yake ni ya vipindi vifupi. (mchoro nambari 2).

**Mchoro Namba 2: Mfumko wa Bei wa Bidhaa Za Chakula na Zisizo za Chakula Julai – Septemba 2020/2023**





***Chanzo:*** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar.

## 1.4 Uingiaji wa Watalii

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2023, idadi ya watalii imeongezeka na kufikia watalii 171,943 ikilinganishwa na wastani wa 165,883 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3.7.

Ongezeko la watalii limetokana na juhudi za Serikali kudumisha amani na utulivu nchini hali inayovutia wageni kutembelea Zanzibar, kuongezeka kwa Mawakala wa Usafirishaji Watalii (Tui- Tourism Union International na African Tours &Travel Companies.); kuitangaza Zanzibar kiutalii kupitia maonyesho ya nje ya nchi; makongamano na matamasha kwa mataifa mbali mbali duniani. Vile vile, mabalozi wa Tanzania waliopo nje ya nchi wameendelea kuutangaza vivutio vya utalii; pamoja na kufunguliwa kwa hoteli za nyota tano ambazo zinauwezo wa kupokea wageni wengi kwa wakati mmoja kama vile Hotel Riu Jambo na Emerald Zanzibar Resort & Spa. (Mchoro namba 3)

**Mchoro namba 3: Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Julai-Septemba 2022-2023.**





**Chanzo:** Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar.

## 1.5 Mwenendo wa Thamani ya Sarafu ya Tanzania

Mwenendo wa thamani ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani ni muhimu kutokana na mauzo na ununuzi bidhaa nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai-Septemba mwaka 2023, Shilingi ya Tanzania imeshuka thamani dhidi ya Dola ya Kimarekani kwa wastani wa TZS 2,415.4 kwa dola moja ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,305.23 kwa Dola moja ya Kimarekani mwaka 2022 sawa na kupungua thamani kwa wastani wa asilimia 4.7. Hii ni kutokana na kupanda kwa Hati Fungani (Treasury Bill) nchini Marekani kulikopelekea kupanda kwa kiwango cha riba na kuwepo kwa mahitaji makubwa ya fedha za kigeni katika ununuaji wa bidhaa kutoka nje. (Mchoro nambari 4).

**Mchoro namba 4: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani**




**Chanzo:** Benki Kuu ya Tanzania (BoT), 2023

kwa upande wa sarafu nyengine, Paundi moja ya Uingereza ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 3,057.9 katika kipindi cha Julai –Septemba mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,713.3 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022. Euro moja ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,628.6 katika kipindi cha Julai - Septemba mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,322.4 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022. Rupia moja ya India ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 29.1 kwa kipindi cha miezi mitatu mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa TZS 28.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Yuan moja ya China ilibadilishwa kwa watani wa TZS 333.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa TZS 336.5 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2022.

## 1.6 Uingizaji na Usafirishaji wa Bidhaa

Kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa ndani ya nchi kumepelekea kuongezeka kwa nakisi ya biashara katika kipindi cha Julai-Septemba 2023 na kufikia thamani ya TZS 374.7 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 305.8 bilioni

kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 22.5.

Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023, thamani ya usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi imepungua na kufikia thamani ya TZS 19.6 bilioni kutoka thamani ya TZS 28.8 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 31.7. Kupungua kwa thamani ya usafirishaji kumetokana na kutokusafirishwa kwa zao la karafuu kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023 kutokana na mabadiliko ya msimu wa zao hilo, pamoja na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa za chakula na wanyama hai kufikia wastani wa thamani ya TZS 15,728.2 milioni kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023 kutoka wastani wa thamani ya TZS 33,036.2 milioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kwa kipindi cha Julai-Septemba 2023, thamani ya uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imeongezeka na kufikia thamani ya TZS 394.3 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 334.6 bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la

asilimia 17.8. Kuongezeka kwa thamani ya uagiziaji katika kipindi cha Julai-Septemba 2023 imetokana na kuongezeka kwa uagiziaji wa bidhaa za mashine na vifaa vya usafiri kufikia wastani wa thamani ya TZS 113,226.2 milioni kutoka wastani wa thamani ya TZS 36,518.5 milioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

### 1.7 Hali ya Chakula

Katika kipindi cha Julai - Septemba, 2023, bidhaa zilizoingizwa nchini kutoka nje ni kama ifuatavyo:

i. Mchele ulioingia nchini tani 19,498 ikilinganishwa na tani 30,747 za kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 36.5 Hii imetokana na Changamoto ya upatikanaji wa dola katika masoko ya ndani, Kupungua kwa mavuno ya mchele wa mapembe Pakistani ambapo wafanyabiasha wananunua kwa wingi, na kufungwa kwa utoaji wa chakula kwa nchi ya India hali iliopelekea mahitaji kuongezeka kwa Nchi nyengine na kusababisha kuongezeka kwa bei katika soko la Dunia;

ii. Tani za sukari zilioingia nchini imefikia tani 4,617 kutoka tani 5,850 za kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 21.0. Kwa mujibu wa shirika la biashara duniani "*World Trade Organisation* "bei ya bidhaa ya sukari ilipanda kwa kipindi cha mwezi Aprili - Mei, 2023 na athari yake imeonekana katika kipindi cha Julai – Septemba;

iii. Unga wa ngano ulioingia nchini umefikia tani 959 kutoka tani 1,195 za kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 19.7. Hii imetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa ndani na kupelekea kupungua kwa uingizaji kutoka nje;

iv. Mafuta ya kula yulioingia nchini yamefikia tani 22,048 kutoka tani 46,984 sawa na upungufu wa asilimia 53.0

Bidhaa zilizoingizwa nchini kutoka Tanzania Bara ni kama ifuatavyo:

i. Mchele ulioingia nchini tani 3,320 ikilinganishwa na tani 779.5 za kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 325.9.

ii. Unga wa ngano ulioingia nchini umefikia tani 1,380 kutoka tani732.75 za kipindi kama hicho mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 88.3. Hii imetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani,

Takwimu zinaonesha tani 12,147.64 za unga wa ngano zimechakatwa kwa kipindi cha Julai–Septemba 2023 kutoka tani 15,078.916 katika kipindi kama hicho mwaka 2022 kwa ajili ya matumizi ya ndani katika kiwanda cha 'Azam Zanzibar Milling' na sukari tani 3,100 zilizalishwa na kiwanda cha Sukari Mahonda. Zanzibar inakadiriwa kutumia wastani wa tani 11,484 za mchele, tani 3,000 za sukari, tani 4,776 za unga wa ngano na tani 544 za mafuta ya kula kwa mwezi. Mafuta ya kula yaliyoingia nchini yamefikia tani 22,048 kutoka tani 46,984 sawa na upungufu wa asilimia 53. Hii ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa dola katika masoko ya ndani na kuongezeka kwa bei katika soko la dunia. **Kiambatisho Nam 1:** Uingizaji wa Bidhaa muhimu za chakula.

### 1.8 Hali ya upatikanaji wa ajira

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, ajira zilizozalishwa hapa Zanzibar kutokana na kutanuka shughuli za kiuchumi zimefikia 4,859. Ajira kutoka sekta ya umma ni 941, sekta binafsi 3,918 ambapo ajira 342 zimetokana na uwekezaji wa miradi mbali mbali nchini. Katika kipindi hichi, miradi 14 iliwekezwa**.** **Kiambatisho Namba: 2** Miradi iliyoorodheshwa na ZIPA kwa kipindi cha Julai-Septemba.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI JULAI-SEPTEMBA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 MAPATO YA SERIKALI

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2023; Serikali ilikadiria kukusanya TZS 548.79 bilioni. Hadi kufikia Septemba 30, 2023 kiasi cha TZS 545.18 bilioni zilikusanywa sawa na asilimia 99.3 ya makadirio ya kipindi hicho. Mapato hayo yanaonesha ukuaji

wa 65.9 ikilinganishwa na mapato ya TZS 328.46 bilioni yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023

### 2.1.1 Mapato ya ndani

Mapato ya ndani yalikadiriwa kufikia TZS 324.79 bilioni ambapo makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai- Septemba yalifikia TZS 325.27 bilioni sawa na asilimia 100.1 kwa makadirio ya kipindi hicho. Mapato yaliyokusanywa katika kipindi cha tathmini yameonesha ukuaji wa asilimia 17 ikilinganishwa na mapato ya TZS 278.46 bilioni yaliyokusanywa kwa kipindi kinachofanana kwa mwaka 2022/2023.

#### i. Mapato kutoka Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imekadiria kukusanya TZS 156.55 bilioni katika kipindi cha Julai hadi Septemba 30, 2023, Mamalaka imefanikiwa kukusanya TZS 161.84 bilioni sawa na asilimia 103.38 ya makadirio ya kipindi hicho. Mapato hayo yameonesha ukuaji wa asilimia 23 ikilinganishwa na TZS 131.85.bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

#### ii. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Upande wa Zanzibar

Kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai- Septemba 2023 Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya TZS 122.47 bilioni na hadi kukamilika kwa robo mwaka, fedha zilizokusanywa zimefikia TZS 115.95 bilioni sawa na asilimia 94.7 ya makadirio ya kipindi hicho. Hata hivyo, mapato hayo yameonesha ukuaji wa asilimia 10 ikilinganishwa na TZS 105.17 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2022/2023. **Kiambatisho Nam 3:** Mchanganuo wa Mapato kwa kianzio.

#### iii. Mapato yasiyokuwa ya kodi

Kwa upande wa mapato yasiyokuwa ya kodi yalikadiriwa kukusanywa TZS 40.52 bilioni ambapo makusanyo halisi kwa kipindi cha Julai Septemba ni TZS 42.24 bilioni sawa na asilimia 104 ya makadirio ya kipindi hicho. Mapato hayo yanaonesha

ukuaji wa asilimia 17 ukilinganisha na mapato ya TZS 36.19 bilioni zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 kutokana na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato hayo. Kwa upande wa kodi ya wafanyakazi wa SMT walioko Zanzibar ilikusanywa kwa asilimia mia moja kama ilivyotarajiwa (TZS 5.25 bilioni).

## 2.2 Mapato Mengineyo

Serikali ilikadiria kukusanya TZS 224 bilioni kwa upande wa mapato mengineyo ambayo yanajumuisha mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Misaada ya Kibajeti na Mikopo ya Serikali kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kukamilika kwa robo ya kwanza mapato hayo yamefikia TZS 219.9 bilioni sawa na asilimia 98.17 ya makadirio ya kipindi hicho. Mapato hayo yameonesha ukuaji wa asilimia 340 ukilinganisha na mapato halisi ya TZS 50 bilioni yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/2023. Ukuaji huu umetokana na Mkakati wa Serikali juu ya Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele katika Miradi ya Kimkakati ambapo Serikali imefanikiwa kupata Mkopo kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi hiyo.

### 2.2.1 Mapato ya Washirika wa Maendeleo

Serikali ilikadiria kupata TZS 26.2 bilioni kutokana na fedha kutoka kwa Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Septemba 30, 2023 TZS 37.1 bilioni zilipatikana, ambapo Mkopo TZS 11.65 sawa na asilimia 44 .4 ya makadirio na TZS 25.45 bilioni ni misaada sawa na asilimia 84.8 ya makadirio ya kipindi hicho .

Mkopo wa TZS 11.65 bilioni ulitumika kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatayo:

i. Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Maji Zanzibar TZS 7.5 bilioni kutoka EXIM Bank
ii. Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Lazima (Ujenzi wa Madarasa Matatu ya Sekondari) TZS 2.68 bilioni kutoka BADEA
iii. Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi mmoja TZS 0.90 bilioni

iv. Mradi wa Uimarishaji wa Afya ya Mama na Mtoto TZS 1.1 bilioni kutoka Benki ya Dunia
v. Mradi wa Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu umepatiwa TZS 0.25 bilioni kutoka AfDB, BADEA na Saudi Fund;

Kwa upande wa Misaada ya TZS 25.45 bilioni zilitumika kwa ajili ya kutekeleza Programu na Miradi mbalimbali, ikiwemo ya afya, uwezeshaji wa wananchi, uimarishaji wa sekta ya sheria na mengineyo kama inavyoonekana katika **kiambatanisho namba 4**

### 2.2.2 Mikopo ya Ndani

Serikali ilikadiria kukopa TZS 197.8 bilioni kutoka vyanzo vya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo hadi kukamilika kwa robo ya kwanza mkopo halisi uliopatikana ni TZS 182 .8 bilioni sawa na asilimia 92.4 ya makadirio ya kipindi hicho. Mikopo hii ilitumika kwa ajili ya Utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. Ujenzi wa Madarasa 1,000 kwa Unguja na Pemba
ii. Ukarabati wa Uwanja wa Amani
iii. Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria- Ras Mkumbuu
iv. Ujenzi wa Barabara za Ndani kilomita 275.09
v. Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar Nyamanzi na Dunga
vi. Ujenzi wa masoko ya Kimkakati Unguja.

## 2.3 MATUMIZI YA SERIKALI

Katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali tuliyoiwasilisha Juni 2023, tulieleza malengo makuu ya Serikali kwa bajeti tuliyoipitisha ni ***"Kuinua Uchumi wa Wananchi wa Zanzibar na Kuimarisha Miundombinu ili Kuvutia Uwekezaji hapa Nchini".*** Katika utekelezaji wa dhana hiyo miongoni mwa maeneo ambayo tuliyapa kipaumbele ni pamoja na kuendelea kugharamia miradi ya kuimarisha Miundombinu ya Barabara, kuimarisha huduma za jamii, Kufanikisha Mkutano wa Mapitio ya Muda wa Kati wa Utekezaleji wa Shughuli za Benki ya Dunia za Kupitia Dirisha la IDA kwa mzunguko wa 20 (IDA-20 Mid Term Review) na

Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mapato yanayotokana na Utalii.

Katika kipindi cha Robo ya kwanza maeneo tuliyoyawasilisha yameshaanza kutekelezwa kwa zaidi ya asilimia 50 na mengine yako katika hatua nzuri ya utekelezaji wake. Mkazo unaendelea kuwekwa katika kugharamia Mipango ya Maendeleo pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa kutumia rasilimali za ndani na Washirika wa Maendeleo wanaendelea kuwa na nafasi ya kusaidia jitihada za Serikali katika utekelezaji wa Mipango yetu.

Kwa upande wa matumizi ya Serikali katika kipindi cha Julai – Septemba ilikadiria kutumia TZS 451.12 bilioni, hadi kufikia Septemba 30, 2023 jumla ya TZS 506.07 bilioni zimetumika sawa na asilimia 112.18 ya makadirio ya kipindi hicho

### 2.3.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida

Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 296.23 bilioni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, hadi kufikia Septemba 30, 2023 kiasi cha TZS 274.93 zimetumika sawa na asilimia 92.8 ya makadirio ya kipindi hicho ambapo matumizi hayo yameelekezwa katika maeneo yafuatayo;

**Mishahara kwa wafanyakazi wa Serikali;**

Kwa upande wa Mishahara ya Wafanyakazi katika kipindi cha Julai-Septemba 30, 2023, makadirio yalikuwa ni TZS 141.62 bilioni hadi kufikia Septemba 30, 2023 kiasi cha TZS 142.42 bilioni kililipwa sawa na asilimia 100.6% ya makadirio.

**Mishahara kwa ajili ya Taasisi za Ruzuku;**

Taasisi za ruzuku katika kipindi cha Julai hadi Septemba 30, 2023 zilikadiriwa kulipa Jumla ya TZS 26.42 bilioni hadi kufikia Septemba 30, 2023 jumla ya TZS 27.57 bilioni zimelipwa ambapo ni sawa na asilimia 104 ya makadirio

**Matumizi mengineyo ya Taasisi za Ruzuku;**

Matumizi mengineyo ya Taasisi za Ruzuku zilikadiriwa kutumika TZS 17.44 bilioni hadi kufikia Septemba 30, 2023 tayari TZS14.69 bilioni zilitumika sawa na asilimia 84.2 ya makadirio ya kipindi hicho.

**Matumizi mengineyo ya Mafungu;**

Jumla ya TZS 50.26 zilipangwa kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Mafungu hadi kufikia Septemba 30, 2023, TZS 24.82 bilioni zilitumika sawa na asilimia 49.4 ya makadirio.

### 2.3.2 Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali

Mfuko Mkuu wa Serikali ulikadiriwa kutumia TZS 60.49 bilioni hadi kufikia Septemba 30, 2023 matumizi ya mfuko huo yamefikia TZS 65.43 bilioni sawa na asilimia 108.17 ya makadirio. Fedha hizo zimetumika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Malipo ya mafao ya Kiinua Mgongo TZS 6.22 bilioni kwa wastaafu 250;
ii. Malipo ya Pencheni Jamii na Pencheni ya wastaafu wa SMZ TZS 15.74 bilioni (Pencheni jamii TZS 4.51 bilioni na Pencheni ya wastaafu TZS 11.23 bilioni)
iii. Malipo ya Mikopo ya ndani na Riba TZS 22.69 bilioni; na
iv. Matumizi ya mengineyo ya Serikali TZS 20.78bilioni

### 2.3.2 Matumizi ya Miradi ya Maendeleo

Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Serikali ilikadiria kutumia TZS 154.89 bilioni hadi kufikia Septemba 30, 2023 kiasi cha TZS 231.14 bilioni sawa na asilimia 149 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Kati ya matumizi hayo, TZS 136.49 bilioni zinatokana na fedha za Ndani sawa na asilimia 134.2 ya makadirio ya TZS 101.69 bilioni kwa kipindi hicho. Aidha, TZS 49.65 bilioni ni Mikopo na Misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Serikali imeanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kuhudumia mikopo ya ndani kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika hatua hiyo, Serikali ilipanga kuweka TZS 27 bilioni kwa ajili ya akiba kwa mwezi wa Julai hadi Septemba 2023, hadi kufikia mwisho wa Mwezi wa Septemba TZS 45 bilioni ziliwekwa kwa ajili ya lengo hilo ambapo sawa na asilimia 166.6 ya makadirio. **Kiambatisho Nam:4**

**Utekelezaji wa Mapato na Matumizi Kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha Julai -Septemba, 2023**

## 2.4 Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha Julai - Septemba makusanyo yamefikia TZS 2.48 bilioni sawa asilimia 67 ya makadirio ya ukusanyaji wa TZS3.68bilioni kwa kipindi hicho. Kwa upande wa matumizi kwa robo ya kwanza jumla ya TZS 2.45 zimetumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mamlaka hizo.

**Kiambatanisho Namba 6** kinaelezea utekelezaji wa Mapato na Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Julai- Septemba 2023:

# 3.0 UTEKELEZAJI MPANGO WA MAENDELEO JULAI – SEPTEMBA 2023

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/24 ni mpango wa tatu wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) (2021-2026) na umelenga kutekelezaji jumla ya 31 (Programu 3 mpya) na miradi ya maendeleo 58 (19 ni miradi mipya). Kiasi cha TZS 1,521.99 bilioni zimepangwa kutumika kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo ambapo TZS 1,514.79 bilioni zitatumika kwa miradi ya maendeleo katika Serikali Kuu na TZS 7.2 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ikiwa ni ongezeko la TZS 162.60 bilioni sawa na asilimia 12.0 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2022/23 ya TZS 1,352.19 bilioni.

## 3.1 Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele kwa Kipindi cha Julai- Septemba 2023

Ili kuhakikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-26) unafanyika kwa ufanisi, miradi ya kimkakati iliweza kutekelezwa ili kuimarisha Ukuzaji wa Uchumi, miundombinu, huduma za jamii na utawala bora.

### 3.1.1 Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu

Katika kuimarisha miundombinu, Serikali katika eneo hili imepanga miradi sita ya kimkakati kama ifuatavyo:

***i.*** **Programu ya Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege- Pemb*a.***

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya kimataifa. Kwa mwaka 2023/2024 programu itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba kwa hatua za awali. Programu itahusisha ujenzi wa maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Programu itagharimu jumla ya TZS.160.0 bilioni. (TZS 10.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 150.0 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya ukamilishaji taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya kuanza mradi imeshakamilika na tathmini imeshafanyika kwa waathirika wa mradi. Hivyo, mradi unasubiri kupata ithibati (No Objection) ili kuweza kuomba fedha za awali na kuanza ujenzi.

**ii. Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani;**

Mradi huu una lengo la kujenga bandari kubwa ya kisasa ambayo itahusisha gati tano ikiwemo gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta, bandari ya uvuvi, pamoja na chelezo cha kukarabati meli, kukamilika kwa ujenzi wa bandari hii kutasaidia kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta uvuvi, biashara na viwanda. Mradi huu ulianza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2022/2023. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na wawekezaji kutoka katika sekta binafsi. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya utengenezaji wa njia kwa upande wa kaskazini kilomita 1.3 tayari imeanza kwa kujazwa kifusi kwa kiwango cha Sub base, kwa upande wa Magharibi urefu wa kilomita 4.4 kifusi tayari kimeshajazwa kwa kiwango cha Sub base na kufikia kilomita 4.25 na ujenzi wa Culvert saba tayari umeshakamilika.

### iii. Kuimarisha bandari za Malindi, Wete na Mkoani;

Mradi wa bandari ya Malindi tayari umeshakamilika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Kwa upande wa bandari ya Wete, hadi kufikia Septemba 2023, kazi ya upembuzi yakinifu na Usanifu wa Awali (Feasibility Study and Preliminary Engineering Design) imekamilika ambapo hatua inayofuata ni kuwasilisha aina ya mchoro utakaotoa mwelekeo wa ujenzi wa Bandari mpya inayohitajika.

Kwa upande wa Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani, hadi kufikia Septemba 2023, ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmong'onyoko wa udongo (Retaining Wall) na kuboresha Gati (Jetty) kwa kuziba nyufa na kurekebisha zege iliyoharibika umefanyika na hatua inayofuata ni kufanya manunuzi ya vitendea kazi kwa ajili ya ushushaji wa makontena na kujenga upya njia ya wapita kwa miguu. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kuhudumia makontena ipasavyo na hatimae kupunguza gharama za bidhaa mbalimbali Pemba.

### iv. Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Programu ya ujenzi wa barabara kuu imeanza mwaka 2022/23 na inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 407.6. Kwa mwaka 2023/2024 programu itahusisha ujenzi wa barabara kuu mbalimbali ikiwemo barabara mpya na zinazoendelea na inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Programu hii ina lengo la kujenga kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani kwa barabara kuu za Unguja na Pemba. Programu itasaidia kwa kiasi kikubwa kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar sambamba na kuhuisha uchumi na uwekezaji kwa vile barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine ya kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 249.38 bilioni (TZS 75.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 174.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Programu hii imejumuisha ujenzi wa barabara ya Tunguu-Makunduchi km 53; ujenzi kwa

barabara ya Chake Chake-Mkoani km 43.5; ujenzi wa barabara ya Fumba - Kisauni kilomita 12 pamoja na Airport spur; na Kuendelea na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake km 22.1. Hadi kufikia Septemba, 2023, kazi ya ukamilishaji taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya kuanza mradi imeshakamilika na tathmini imeshafanyika kwa waathirika wa mradi. Hivyo, mradi unasubiri kupata ithibati (No Objection) ili kuweza kuomba fedha za awali (Advance Payment) na kuanza ujenzi.

### v. Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani

Programu hii imeanza mwaka 2022/2023 na itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Programu itasaidia kuunganisha mitaa na maeneo 62. Aidha, kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha mitaa na maeneo mbalimbali. Vile vile programu itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mzigo na kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu imepangiwa jumla ya TZS 44.0 billioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya uwekaji wa lami na kifusi kwa barabara za Unguja na Pemba inaendelea na utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 31.5.

### vi. Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

Programu hii imeanza kutekelezwa mwaka 2022/2023 na imehusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini. Kwa mwaka 2023/2024 programu hii itahusisha uimarishaji wa barabara kadhaa katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na itahusisha ujenzi wa barabara, ujenzi wa njia za wapita kwa miguu, uwekaji wa taa pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji katika barabara za mijini. Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha miji yetu na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara.

**Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, programu imepangiwa jumla ya TZS 80.1 kutoka Serikalini.** Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya matengenezo ya barabara ya K/Samaki Junction Amani - Mtoni Junction Mkapa Road km 8.5 ujenzi umeanza kwa usafishaji wa njia na uwekaji wa fusi tabaka la tatu utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 23.

Kwa upande wa Ujenzi wa barabara ya Abeid Amani Karume Airport – Kiinua Miguu – Magereza – Mnazimmoja ujenzi umekamilika kwa asilimia 90 kwa km 6.5. Aidha, Barabara ya Chukwani mwisho – Buyu utekelezaji umefikia asilimia 75, barabara ya Msumbiji kinyang'unya – Mwanakwerekwe kazi imekamilika kwa asilimia 93.

Kwa upande wa barabara ya Mazizini Vitambulisho – Zanzibar beach resort – Fish Market utekelezaji umefikia asilimia 52, barabara ya Mwanakwerekwe Gapco – Kwerekwe Skuli – kanisani kwamchina utekelezaji umefikia asilimia 68, barabara ya Mombasa Panned Area km 6.20 kazi imeanza na imefikia asilimia 19 na kwa barabara ya Michenzani, Gongoni, Kisiwandui Msikiti Mabati - Hailesalasie matengenezo yameanza na utekelezaji wake umefikia asilimia 60. Gharama zilizotumika hadi sasa ni TZS 21.34 bilioni

### vii. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka sita (2022-2027) na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 372.48 bilioni kwa lengo la kuimarisha utekelezaji katika sekta ya nishati kwa kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2023/2024, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.08 bilioni (TZS 7.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.88 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya kuandaa michoro na kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa laini ya mkondo mkubwa wa umeme yenye uwezo wa kilovolti 132 imefanyika.

### 3.1.2 Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii

Katika uimarishaji wa huduma za kijamii Serikali imekusudia kuimarisha Sekta ya Elimu, Afya, Michezo, Miundombinu ya usambazaji maji safi pamoja na kutilia mkazo Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (BIG-Z). Serikali katika eneo hili imepanga miradi sita ya kimkakati kama ifuatavyo:

**viii. Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo;**

Mradi wa ujenzi wa Viwanja vya michezo vidogo vidogo (6-in-1 multi-sports Centre) una lengo la kukuza usawa wa kijinsia pamoja na kubadilisha fikra na mifumo ya tabia kuhusu udhalilishaji wa wanawake na watoto. Kukuza uwezo wao kibinafsi na kijamii na kuhamasishwa juu ya usawa wa kijinsia na ushirikishwaji kwa vijana, wanawake na watoto. Mradi huu utahusisha viwanja vinne (Unguja 2 na Pemba 2) vyenye hadhi ya kisasa vitakavyojengwa katika maeneo ya Mkokotoni na SUZA kwa Unguja na Mchangamdogo na Kangani kwa Pemba. Viwanja hivyo vitajumuisha michezo ya basketball, handball, baseball, vollyball na netball

Mradi huu utagharimu jumla ya TZS 1.28 bilioni kutoka Shirika la Kimataifa la Marekani (GIZ). Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya kutangazwa zabuni ya ujenzi wa viwanja vinne imefanyika.

Ukarabati wa uwanja wa Amani unaendelea vizuri. Kazi zilizofanyika kuweka miundo mbinu ya Maji, Umeme, Ukarabati wa jengo la Hoteli, uwekaji wa majukwaa ya kukalia VIP na majukwaa ya kawaida, kufunga viti kwenye majukwaa, kupaka rangi kwenye majukwaa, kufunga masinki ya vyoo, uwekaji wa vioo kwenye vyoo, ujenzi wa maduka, nguzo za mapaa, ujenzi wa mabanda ya mikahawa na maduka, ujenzi wa ukumbi wa judo, ujenzi wa viwanja vya ndani vidogo vidogo (Indoor facilities), Ujenzi wa viwanja viwili vya mpira wa miguu. Mpaka sasa hivi jumla TZS 45.00 bilioni zimetumika.

**ix. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa**

Programu ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili wawe na utulivu wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi na kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, TZS 20.0 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa programu hii. Programu hii imejumuisha Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika hospitali ya Mkoa –Lumumba; hospitali ya Wilaya – Pangatupu; hospitali ya Wilaya - Mwera Pongwe; hospitali ya Wilaya – Kitogani; hospitali ya Wilaya – Vitongoji; na hospitali ya Wilaya – Kinyasini. Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa nyumba hizo katika hospitali 5 za wilaya umefanyika na kwa upande wa Hospitali ya Mkoa –Lumumba mchakato uliotumika ni kutumia njia ya 'Restricted Tendering'.

**x. Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Binguni;**

Kwa upande wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa Binguni hadi kufikia Septemba 2023, upembuzi yakinifu umekamilika na maombi ya fedha yamekamilika ambapo tayari mchakato umeanza wa Wizara ya Fedha.

**xi. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Elimu;**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunza. Kwa mwaka 2023/2024 Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 131.23 bilioni (TZS 59.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 72.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Septemba, 2023 ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Mkokotoni umefikia asilimia 85, Skuli ya Sekondari ya Kijichi utekelezaji umefikia asilimia 60, Skuli ya Msingi ya Donge utekelezaji umefikia asilimia 60, na Skuli ya Msingi ya Maungani utekelezaji umefikia asilimia 20.

**xii. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)**

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar inalenga kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Programu hii inatekelezwa

kwa kipindi cha miaka mitano (2021- 2026) kwa gharama za jumla ya TZS 346.5 bilioni. Kwa mwaka 2023/2024, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 22.810 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba imefanyika na Kampuni zilizoshinda kusambaza vifaa hivyo tayari zimeshajulishwa. Vile vile, kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa urithi wa kihistoria ya Mji Mkongwe (Green Corridor) tayari Ofisi ya mradi imeshafanya kikao cha maridhiano (negotiation meeting) kabla ya kufunga mkataba na kampuni iliyoshinda zabuni.

### 3.1.3 Utawala bora na Uhimilivu

Katika kuimarisha Utawala bora na Uhimilivu, Serikali katika eneo hili imepanga kutekeleza miradi miwili kama ifuatavyo:-

#### i. Mradi wa kuimarisha Ulinzi na Usalama

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi kwa kufikia viwango vya kimataifa ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 na utagharimu jumla ya TZS 31.09 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2023/2024 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza shughuli za kuweka miundombinu mipya ya mawasiliano ya ulinzi na usalama; ununuzi wa vitendea kazi vya operesheni vya Idara Maalum za SMZ; na kusimamia uendeshaji wa Mradi wa Mji Salama. Hadi kufikia Septemba, 2023 mkataba wa manunuzi ya vifaa tayari umeshasainiwa na hatua za malipo zinaendelea.

#### ii. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar

Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Programu imepanga kujenga Ofisi mpya katika maeneo ambayo yamependekezwa na Serikali na kukarabati majengo ambayo yameonekana kuchakaa au kupungua nafasi katika Ofisi hizo. **Kwa mwaka 2023/2024, program imepangiwa jumla ya**

**TZS74.12 bilioni** kutoka Serikalini. Serikali itajenga Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka na jumla ya TZS 55.0 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia ujenzi huo kwa hatua za awali. Aidha, Serikali inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa majengo na ofisi za Serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya majengo ili kuleta haiba ya miji, jumla ya TZS 19.0 bilioni zimepangwa na kuanza kutumika kugharamia ujenzi wa majengo mbali mbali ya Serikali yakiwemo Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA) Maruhubi, Tume ya Uchaguzi na Shirika la Nyumba.

Hadi kufikia Septemba, 2023 kazi ya kujenga ghorofa ya kwanza, usimamishaji wa nguzo na viambaza pamoja na uwekaji wa zege na uwekaji wa plasta katika jengo la Ofisi ya Mufti imefanyika.

### 3.2 Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai -Septemba 2023/2024

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miezi mitatu (Julai-Septemba) kwa robo ya kwanza ni pamoja na:

i. Kupatikana kwa miundombinu ya barabara ambayo inarahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu na kuunganisha mikoa yote;
ii. Kuendelea kwa kiwango cha kuridhisha cha utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo;
iii. Kupatikana kwa huduma za kiuchumi na kijamii kwa programu na miradi iliyokamilika; kwa haraka na kwa muda muafaka.

### 3.3 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2023/24

Licha ya mafanikio yaliyopatikana katika maeneo yote ya kimkakati yaliyoelezewa hapo juu, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Kukosekana kwa mawasiliano na ushirikiano wa kutosha baina ya watekelezaji wa mradi na maafisa Ufuatiliaji wa sekta husika;

ii. Kutokufanya kazi kwa timu ya pamoja ya wataalamu wanaosimamia sekta za miundombinu zinazotekelezwa sambamba;
iii. Kukosekana kwa usimamizi wa vihatarishi (Risk Management), uhifadhi wa mazingira pamoja na mabadiliko ya tabia nchi katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo;
iv. Kutokuridhisha kwa kasi ya utekelezaji kwa baadhi ya Programu na Miradi ya Maendeleo;
v. Upatikanaji hafifu wa rasilimali za kufanyia kazi za Ufuatiliaji na Tathmini kwa Miradi ya Maendeleo.


## 4.0 DENI LA TAIFA

Deni linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hadi kufikia Septemba 2023, limefikia TZS 518.04 bilioni ambapo kati ya deni hilo, deni la ndani ni TZS 503.81 bilioni sawa na asilimia 97.3 ya deni lote na deni la nje ni TZS 14.23 bilioni sawa na asilimia 2.7, ukilinganisha na deni lililodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar la mwezi Septemba 2022 ambapo lilifikia TZS 333.61 bilioni ambapo kati ya deni hilo, deni la ndani lilikua TZS 320.37 bilioni sawa na asilimia 96 ya deni lote na deni la nje lilikua ni TZS 13.24 bilioni sawa na asilimia 4 ya deni lote.

**Jadweli Namba:1 Uchambuzi wa Deni kwa Mwezi Septemba 2023 na Septemba 2022**

| **DENI** | **SEPTEMBA 2023** | **SEPTEMBA 2022** |
|---|---|---|
| Deni la Ndani | 503.81 | 320.37 |
| Deni la Nje | 14.23 | 13.24 |
| **JUMLA** | **518.01** | **333.61** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali





Kati ya deni la TZS 503.81 bilioni kwa mwezi Septemba 2023, hati fungani za muda mrefu ambazo zimechukuliwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania ni TZS 267.85 bilioni sawa na asilimia 53.11, deni ambalo limechukuliwa kutoka ZSSF ni TZS 33.52 bilioni sawa na asilimia 6.76, deni kutoka PBZ ni TZS 27.00 bilioni sawa na asilimia 5.35 na deni kutoka NBC ni TZS 175.44 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 34.78 ya deni lote.

Ukilinganisha na deni la TZS 320.37 bilioni kwa mwezi Septemba 2022, hati fungani za muda mrefu ambazo zilichukuliwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania ni TZS 279.52 bilioni sawa na asilimia 87.2, deni ambalo limechukuliwa kutoka ZSSF ni TZS 40.85 bilioni sawa na asilimia 12.8 ya deni lote.

**Jadweli Namba:2 Mlinganisho wa Uchambuzi wa Deni kwa Taasisi**

| **Deni** | **Septemba 2023** | **Septemba 2022** |
|---|---|---|
| BENKI KUU (BOT) | 267.85 | 279.52 |
| ZSSF | 33.52 | 40.85 |
| PBZ | 27.00 | 0.00 |
| NBC | 175.44 | 0.00 |
| **JUMLA** | **503.81** | **320.37** |

**Chanzo:** Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali




Hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2023 Deni la Nje linalodhaminiwa na SMT kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,525.29 bilioni sawa na USD 1,017.54, tofauti na deni la tarehe 30 Septemba 2022 ambapo Deni la Nje linalodhaminiwa na SMT kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar lilifikia TZS 2,327.36 bilioni sawa na USD 1,008.41.

## 6.0 VIAMBATISHO

**Kiambatisho Nam I:** Uingizaji wa Bidhaa muhimu za chakula Kwa kipindi cha Julai-Septemba, 2022/2023.

| Bidhaa/ Tani | Mwaka | Bidhaa kutoka Nje ya Nchi | Bidhaa kutoka Tanzania-Bara | Bidhaa zilizozalishwa Nchini | Jumla ya Bidhaa |
|---|---|---|---|---|---|
| Mchele | 2022 | 30,747 | 779.5 | 0 | 31,526.50 |
| | 2023 | 19,498 | 3,320 | 0 | 22,818 |
| Unga wa Ngano | 2022 | 1,195 | 732.75 | 15,078.90 | 17,006.66 |
| | 2023 | 959 | 1,380 | 12,147.64 | 14,486.64 |
| Sukari | 2022 | 5,850 | 0 | 0 | 5,850 |
| | 2023 | 4,617 | 0 | 3,100 | 7,717 |
| Mafuta ya kula | 2022 | 46,984 | 0 | 0 | 46,984 |
| | 2023 | 22,048 | 0 | 0 | 22,048 |

**Chanzo:** Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Zanzibar

**Kiambatisho Namba 2:** Miradi iliyorodheshwa na ZIPA kwa kipindi cha Julai-Septemba

| Miradi | Namba ya mradi | Hali ya ajira |
|---|---|---|
| Kilimo,Misitu, na Uvuvi | 1 | 10 |
| Uzalishaji Viwandani | 2 | 39 |
| Huduma za Malazi na chakula | 2 | 90 |
| Ukodishaji majengo | 8 | 203 |
| Sanaa, Burudani na Ubunifu | 1 | 10 |
| Jumla | 14 | 352 |

**Chanzo:** ZIPA

| Jadweli Namba:3 Utekelezaji wa Mapato ya Kodi na Yasiyokuwa ya Kodi kwa Vianzio | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Revenue for the Fiscal Year 2023/2024** | | | | |
| TAX ITEMS | Budget 2023/2024 | TOTAL | | |
| | | Target (July-Sept, 2023) | Actual (July-Sept, 2023) | Perf |
| TOTAL DOMESTIC REVENUE | 1,419,027,138,952 | 322,413,279,232 | 324,619,787,191 | 100.7% |
| TOTAL TAX REVENUE | 1,217,245,240,698 | 281,895,279,232 | 282,380,787,191 | 100.2% |
| TAX REVENUE FROM TRA | 520,643,978,630 | 119,829,983,611 | 115,299,843,350 | 96.2% |
| TAX REVENUE FROM ZRA | 675,601,262,068 | 156,815,295,621 | 161,830,943,841 | 103.2% |
| PAYE (TRANSFER) | 21,000,000,000 | 5,250,000,000 | 5,250,000,000 | 100.0% |
| NON TAX REVENUE | 201,781,898,254 | 40,518,000,000 | 42,239,000,000 | 104.2% |
| CUSTOM DEPTARMENT (TRA) | | | | |
| Import duty | 110,656,206,801 | 27,241,668,047 | 23,320,171,533 | 85.6% |
| Excise Duty Import | 18,013,801,107 | 4,426,092,111 | 6,691,574,133 | 151.2% |
| Excise Duty Petrol | 15,440,400,949 | 3,793,793,238 | 2,981,386,919 | 78.6% |
| VAT Import | 105,509,406,485 | 26,345,021,283 | 21,296,357,947 | 80.8% |
| Infrasctructure Tax (TRA) | 1749912108 | 429,963,233.62 | 591,020,940.67 | 137.5% |
| Fine on import | 617,616,038 | 102,698,687 | 955,699,788 | 930.6% |
| Miscellaneous Custom Fee | 2,521,932,155 | 619,652,896 | 1,372,857,404 | 221.6% |
| Cross Boader Declaration Fee | 257,340,016 | 63,229,887 | - | 0.0% |
| M/Vehicle Levy | 2,573,400,158 | 632,298,873 | 17,651,606 | 2.8% |
| SUB TOTAL | 257,340,015,817 | 63,654,418,254 | 57,226,720,271 | 89.90% |
| DOMESTIC REVENUE DEPARTMENT (TRA) | | | | |
| PAYE | 116,029,320,545 | 24,542,439,132 | 26,497,529,610 | 108.0% |
| Skill Development Levy | 17,347,371,002 | 4,364,920,969 | 3,825,672,527 | 87.6% |
| Corporate | 67,791,879,852 | 15,296,276,472 | 12,085,153,627 | 79.0% |
| Individual | 3,279,014,679 | 901,626,201 | 500,919,531 | 55.6% |
| Excise Duty on LMG | 1,188,218,106 | 196,185,068 | 238,321,332 | 121.5% |
| Withholding Tax-IRMD | 57,668,158,628 | 10,874,117,513 | 14,925,526,451 | 137.3% |
| SUB TOTAL | 263,303,962,813 | 56,175,565,357 | 58,073,123,079 | 103.4% |
| ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY | | | | |
| VAT Local | 355,784,115,403 | 77,849,207,129 | 79,228,865,206 | 101.8% |
| Excise Duty - Service | 37,716,145,428 | 9,855,433,323 | 10,947,838,920 | 111.1% |
| Hotel Levy | 10,865,566,024 | 2,376,881,713 | 2,146,455,633 | 90.3% |
| Restaurant Levy | 3,638,701,180 | 877,607,577 | 571,743,538 | 65.1% |
| Tour Operation Levy | 4,122,625,452 | 475,327,002 | 556,187,046 | 117.0% |
| Stamp Duty | 13,906,557,874 | 3,887,619,983 | 3,175,772,301 | 81.7% |
| Airport Service Charge | 71,552,153,185 | 15,609,912,620 | 18,406,687,170 | 117.9% |
| Seaport Service Charge | 5,826,025,717 | 979,375,273 | 764,920,900 | 78.1% |
| Seaport Transport Charge | 5,595,608,733 | 1,036,588,123 | 917,047,442 | 88.5% |
| Land Lease | 15,818,902,472 | 1,752,155,023 | 1,957,515,329 | 111.7% |
| Road Development Fund | 24,187,133,006 | 5,153,365,299 | 4,312,779,900 | 83.7% |
| Petroleum Levy | 59,012,258,809 | 15,990,128,695 | 15,774,107,951 | 98.6% |
| Motor Vehicle Registration Fees | 4,578,176,887 | 665,787,368 | 616,973,109 | 92.7% |
| Motor Licencing Fees / Road Licence | 3,797,755,884 | 1,953,512,402 | 1,619,046,350 | 82.9% |
| Driving Licence Fees | 3,570,805,387 | 442,352,875 | 413,275,009 | 93.4% |
| Airport Safety Fee | 18,049,469,610 | 3,755,226,831 | 4,220,516,663 | 112.4% |
| Infrasctructure Tax (ZRA) | 23,120,931,238 | 12,475,610,385 | 14,081,991,640 | 112.9% |
| SUB TOTAL | 661,142,932,289 | 155,136,091,621 | 159,711,724,108 | 102.9% |
| Government Levy Mobile Money Transfer | 14,458,329,779 | 1,679,204,000 | 2,119,219,732 | 126.2% |
| SUB TOTAL | 14,458,329,779 | 1,679,204,000 | 2,119,219,732 | 126.2% |
| SUB TOTAL (ZRA) | 675,601,262,068 | 156,815,295,621 | 161,830,943,841 | 103.2% |
| NON TAX REVENUE | | | | |
| MDA's collection | 153,281,898,254 | 40,518,000,000 | 42,239,000,000 | 104.2% |
| Divident from Governemnt Parastals | 35,000,000,000 | | | |
| Divident from BOT | 13,500,000,000 | | | |
| SUB TOTAL | 201,781,898,254 | 40,518,000,000 | 42,239,000,000 | 104.2% |

| **Kiambatisho Namba:4** Fedha za Misaada kutoka Washirika wa Maendeleo kwa kipindi cha Julai- Septemba | | |
|---|---|---|
| **Mradi** | **Mhisani** | **TZS milioni** |
| Mradi wa Ushiriki wa Vijana na Stadi za Maisha | UNFPA | 18.19 |
| Mradi wa Ukimwi kwa Vijana | UNICEF | 19.92 |
| Programu ya Afya ya Uzazi | UNFPA/GF | 154.89 |
| TASAF | World Bank | 7,608.98 |
| Programu ya Mwitikio wa kijinsia, utoaji wa huduma ya haki kwa wanawake kusaidia kesi ya unyanyasaji Zanzibar | UN-Women | 163.41 |
| Uwezeshaji wa Kisheria Kukuza Upatikanaji wa Haki-PHASE II (LEAP II) | UND | 300.59 |
| Programu mmalimbali za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | SMT/UNICEF/BOT/ NBS(SMT) | 970.84 |
| Mpango wa Elimu kwa Watoto Wote wa Nje ya Shule Zanzibar (OOSC) | Qatar/UNICEF | 12.77 |
| Kuimarisha Elimu ya Awali, Msingi na Jumuishi GPE II | GPE | 7.74 |
| Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP) | USAID/Global Fund | 1,769.32 |
| Mradi shirikishi wa kuthibiti Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi,TB & Ukoma | AMREF | 427.61 |
| Programu ya Afya ya Uzazi na Mtoto (IRCHP) | GAVI | 302.47 |
| Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxing Contamination TZS milioni kutoka | AfDB | 1,838.37 |
| Ujenzi wa Mradi wa Umwagiliaji Zanzibar TZS 1,838.37 milioni kutoka | Korea | 11,481.56 |
| Implementing Sterile Technique as Part of Area Wide Intergrated Pest Management | IAEA | 375.83 |
| **Jumla** | | **25,452.49** |

**Kiambatisho Namba. 5 Utekelezaji wa Mapato na matumizi kwa Kipindi cha Julai -Septemba 2023**

| MAPATO | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **ITEMS** | **2022/2023** | **2023/2024** | | | |
| **Maelezo** | **Halisi Julai-Septemba 2022/2023** | **Bajeti 2023/2024** | **Mkadirio Julai Septemba 2023/2024** | **Halisi Julai Septemba2 023/2024** | **Asilimia** |
| ***Mapato ya Ndani*** | ***278.46*** | ***1,419.03*** | ***324.79*** | ***325.28*** | ***100.15*** |
| ZRA | 131.85 | 675.60 | 156.55 | 161.84 | ***103.38*** |
| TRA | 105.17 | 520.64 | 122.47 | 115.95 | ***94.68*** |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 36.19 | 201.79 | 40.52 | 42.24 | ***104.24*** |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 5.25 | 21.00 | 5.25 | 5.25 | ***100.00*** |
| ***Other Revenue*** | ***50.00*** | ***1,403.82*** | ***224.00*** | ***219.90*** | ***98.17*** |
| Mikopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo | | 567.21 | 197.80 | 182.80 | ***92.42*** |
| Mkopo wa ndani /TB | | 150.00 | | | |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | - | 0.24 | - | | |
| Misaada Kutoka Nje | 12.41 | 104.94 | 30.00 | 25.45 | ***84.83*** |
| Mkopo kutoka Nje | 21.85 | 529.24 | 26.20 | 11.65 | ***44.46*** |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 15.74 | 52.19 | - | | |
| **Jumla Kuu** | **328.46** | **2,822.85** | **548.79** | **545.18** | **99.34** |

| MATUMIZI | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2022/2023** | **2023/2024** | | | |
| **ITEMS** | **Halisi Julai-Septemb** | **BAJETI 2023/24** | **Makadirio Julai Septemba** | **Halisi Julai Septemba** | **Asilimia** |
| ***Matumizi ya Kawaida*** | ***223.89*** | ***1,308.06*** | ***296.23*** | ***274.93*** | ***92.81*** |
| Mshahara Mawizara | 125.03 | 631.41 | 141.62 | 142.42 | *100.56* |
| Mshahara Ruzuku | 23.37 | 97.99 | 26.42 | 27.57 | *104.35* |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 26.31 | 236.94 | 50.26 | 24.82 | *49.38* |
| Matumizi Mengeniyo Ruzuku | 9.00 | 85.72 | 17.44 | 14.69 | *84.23* |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 40.18 | 256.00 | 60.49 | 65.43 | *108.17* |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **61.49** | **1,514.79** | **154.89** | **231.14** | **149.23** |
| Fedha za Serikali | 27.60 | 742.00 | 101.69 | 136.49 | *134.22* |
| Mfuko wa Kugharamia Madeni ya Miradi ya Maendeleo (Debt Services Fund) | 0 | 144.00 | 27.00 | 45.00 | *166.67* |
| Misaada Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 0 | 99.55 | 26.20 | 14.25 | *54.37* |
| Mikopo Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo | 33.89 | 529.24 | - | 35.41 | - |
| **Jumla Kuu** | **285.38** | **2,822.85** | **451.12** | **506.07** | **112.18** |

***Chanzo:*** *OR- Fedha na Mipango*

| **Kiambatisho Namba :6 Utekelezaji wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Julai- Septemba** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **SN** | **Taasisi** | **Makadirio ya Mapato Julai-Septemba** | **Mapato Halisi Julai -Septemba** | **Asilimia** | **Matumizi** |
| 1 | Baraza la Manispaa Mjini | 1,061,746,000 | 708,773,503 | 67 | 686,729,539.05 |
| 2 | Baraza la Manispaa Magharibi 'A' | 435,148,750 | 385,474,533 | 89 | 360,858,000 |
| 3 | Baraza la Manispaa Magharibi 'B' | 651,420,000 | 470,673,890 | 72 | 414,198,124 |
| 4 | Baraza la Manispaa Kaskazini 'A' | 311,462,401 | 255,294,353 | 82 | 231,476,592.62 |
| 5 | Baraza la Mji Kaskazini 'B' | 258,893,250 | 162,727,575 | 63 | 280,921,524.65 |
| 6 | Baraza la Mji Kati | 304,448,000 | 106,475,980 | 35 | 97,865,908 |
| 7 | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini | 104,783,334 | 93,367,180 | 89 | 71,177,770.00 |
| 8 | Baraza la Manispaa Chakechake | 156,999,999 | 79,471,320 | 51 | 102,216,890 |
| 9 | Baraza la Mji Mkoani | 243,829,050.00 | 132,291,632 | 54 | 119,244,104 |
| 10 | Baraza la Mji Wete | 98,126,500 | 49,536,484 | 50.5 | 49,536,484 |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | 60,360,000 | 42,303,168 | 70 | 42,303,168 |
| | **JUMLA KUU** | **3,687,217,284** | **2,486,389,618** | **67** | **2,456,528,104.32** |